# Karatasi ya Ukweli ya Sensa ya Australia ya Maendeleo ya Awali (AEDC)

## Kukusanya, Kulinda na Kutumia Data za AEDC

### Taarifa gani inakusanywa?

Data zilizokusanywa kama sehemu ya AEDC zitajumuisha taarifa ya kibinafsi kuhusu mtoto wako, ikiwa pamoja na majina, anwani, asili ya kitamaduni na kilugha na taarifa juu ya afya yake. Taarifa hizi zinaweza kuchukuliwa kutoka rekodi za shule, ili kusaidia waalimu kukamilisha AEDC.

Wakati wa kujaza AEDC, waalimu wanaweza kusaidiwa na washauri wa kitamaduni ambao ni wafanyakazi au wakandarasi wa shule yetu na inaweza kuwasaidia kuelewa muktadha wa kitamaduni wa watoto wa Mataifa ya Kwanza.

### Data za AEDC husimamiwaje?

AEDC inasimamiwa kulingana na Kanuni za Faragha za Australia (Australian Privacy Principles (APPs)). APPs hudhibiti ukusanyaji, matumizi, ufichuzi na uhifadhi wa taarifa za kibinafsi na mashirika ya serikali ya Australia, na baadhi ya mashirika ya sekta binafsi, na ni sehemu ya *Sheria ya Ufaragha ya* 1998 (*Privacy Act 1998* (Cth)).

Taarifa za kibinafsi kuhusu mtoto wako zitatumiwa kuunganisha data za AEDC pamoja na taarifa kutoka mashirika mengine, kama vile idara za afya, ambayo yataziweka siri. Matokeo ya AEDC ya mtoto wako zitawekwa tofauti na taarifa zake za kumtambulisha na hakuna mtu atakayeweza kufikia zote mbili kwa wakati mmoja.

Matokeo ya AEDC kwa watoto binafsi haziripotiwi, na data zote za AEDC zilizochapishwa hazijajulikana, ikimaanisha kuwa majina, umri, anwani na maelezo mengine ya utambuzi huondolewa kabla ya data kuchapishwa.

Unaweza kuona jinsi data inavyokusanywa na kuwasilishwa kwa kutembelea kwa www.aedc.gov.au/data Data kutoka ukusanyaji wa 2024 zitawasilishwa kwa njia sawa.

### Data za AEDC hushikiriwa na nani na jinsi gani zinazoshirikiwa?

#### Shule

Shule zinazostahiki hupokea muhtasari wa matokeo ya AEDC katika mfumo wa wasifu wa shule. Wasifu wa shule hauripoti matokeo yoyote ya AEDC kuhusu mtoto mmoja mmoja.

Shule zinaweza kushiriki wasifu wao na mashirika mengine au watu wengine kwa siri kwa madhumuni kama vile kusaidia watoto vyema, lakini haziwezi kufichua wasifu kwa umma. Ili kulinda zaidi faragha ya watoto, shule zenye watoto chini ya sita wanaoshiriki katika AEDC hazitapokea wasifu wa shule.

#### Mashirika makuu ya serikali na sekta za shule

Idara za serikali za Jimbo na Wilaya na mashirika makuu ya shule za Kikatoliki na Kujitegemea zitapokea taarifa bila majina kwa watoto wote katika sekta ya shule zao.

#### Kuunganisha mamlaka na vitengo vya kuunganisha data

Mashirika yaliyochaguliwa yatapokea taarifa za kibinafsi kuhusu watoto wanaoshiriki katika AEDC ili kuunganisha matokeo ya AEDC pamoja na data zingine. Kulingana na mbinu zinazotumika kwa uunganisho wa data, wanaweza pia kupokea matokeo ya AEDC. Mashirika haya ni pamoja na mashirika ya Jumuiya ya Madola, serikali za Jimbo na Wilaya, vyuo vikuu na taasisi za utafiti ambazo zimeonyesha kuwa na mifumo salama ya kutosha kulinda faragha ya watoto.

#### Watafiti

Watafiti wanaweza kuomba data AEDC bila majina, na data za AEDC zinazoungahishwa na data nyingine ili kujibu maswali ya utafiti. Kuona mifano kuhusu jinsi watafiti walivyotumia data za AEDC tembelea kwa https://www.aedc.gov.au/snapshots

Data za AEDC zisizojulikana pia hushirikiwa na taasisi za utafiti zinazochangia mpango wa AEDC. Katika baadhi ya matukio, data zisizojulikana zinaweza kutolewa kwa taasisi za utafiti za nje.

#### Wakala wa Kusimamia Data wa AEDC

Taarifa za kibinafsi na matokeo ya AEDC ambayo hayakujulikana yanawekwa na kudhibitiwa kwa niaba ya Idara ya Elimu ya Serikali ya Australia na Wakala ulioteuliwa wa Kusimamia Data. Wakala wa Kusimamia Data wa AEDC huchaguliwa kwa uangalifu ili kuhakikisha kwamba data za AEDC hudhibitiwa kwa mujibu wa viwango vya juu zaidi vya usalama. Wakala wa sasa wa Kusimamia Data wa AEDC ni Kituo cha Utafiti wa Kijamii.